

SWALI: Silaha za Nuru ni zipi?

Warumi 13:12 Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru

JIBU: Ni lazima tufahamu ulimwengu wa roho upo katika pande mbili,

1. Upande wa nuru
2. na upande wa giza..

Upande wa Nuru ni wa Kristo (Yohana 1:4-5), na upande wa giza ni wa ibilisi.

Na pande hizi hazijawahi kupatana hata kidogo, na kama hazijawahi kupatana maana yake zipo vitani na kama zipo vitani basi zina silaha zake, kuhakikisha zinajilinda, lakini pia kushambulia, ili kuua utawala mwingine. Ndio hapo kwanini tunaambiwa tuzivae silaha za nuru. Maana yake mtu anaweza akawa ni wa nuru lakini akawa hana/hajui kuzitumia silaha za Nuru.

Vifungu vifuatavyo ni kututhibitishia kuwa Nuru na giza viro katika mapambano;

2Wakorintho 6:14 Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?

Wakolosai 1:12 mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru.

13 Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake

Sasa silaha za Nuru ambazo mtu akiwa nazo atawezeku kujilinda na mashambulizi ya giza, lakini pia atawezeku kuushinda ufalme wa giza ni hizi;

1. **Neno la Mungu.**
2. **Haki (Ya Mungu katika Kristo Yesu)**
3. **Kweli (Usahihi wa kimaandiko)**
4. **Utakatifu**
5. **Imani**
6. **Injili**
7. **Maombi**

Silaha hizi, ndio zile zinazotajwa pia kwenye Waefeso 6:10-18, kama silaha za haki.

- **Kweli Kiunoni**
- **Dirii ya Haki kifuani**
- **Ngao ya Imani**
- **Upanga wa Roho**
- **Utayari wa injili ya Amani**
- **Sala na Maombi**
- **Chapeo ya wokovu**

Kwa maelezo marefu juu ya silaha hizi, fungua hapa usome >>> **Nini maana ya Dirii, Chapeo na Utayari?**

Mtu akiwa na mambo haya, ataweza kulishinda Giza, kotekote.. Ambalo, silaha zake ni kama zifuatazo;

1. **Uongo:** Ambao huzaa Mafundisho ya uongo,
2. **Uasherati:** Uzinzi, tamaa ya macho,
3. **Majivuno :** Ambayo hupelekea uasi,
4. **Chuki :** Huzaa Kutokusamehe, unafki, migawanyo
5. **Hofu :** mashaka, kupoteza imani na Mungu
6. **Uchawi na uganga:** Huzaa ibada za sanamu, miungu, na uvamizi wa mapepo

Swali ni Je! Umejivika silaha Nuru ?

Ikiwa upo nje ya Kristo, huwezi kusimama, unahitaji wokovu kwanza, ikiwa upo tayari kufanya hivyo wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge

Silaha za Nuru ni zipi? (Warumi 13:12)

na channel yetu kwa kubofya link hii

>> <https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Silaha za Mkono wa kuume na za mkono wa kushoto ni zipi

Je mapepo yanakufa? Na kama hayafi, tunashindanaje vita vya kiroho?

NGUVU YA “KUKATAA” UNAPOAMBANA VITA VYA KIROHO

Share on:

WhatsApp